## Maswali

1. Naamani alikuwa nani?
2. Naamani alikuwa na ugonjwa gani?
3. Msichana mtumwa aliambia mke wa Naamani nini?
4. Mfalme wa Israeli alisema nini Naamani alipoenda kumuona?
5. Elisha aliambia Naamani afanye nini?
6. Naamani alifanya nini aliposikia ujumbe wa Elisha?
7. Watumishi wa Naamani walimwambia nini?
8. Nini ilifanyika Naamani alipooga mara 7 kwa maji ya Mto wa Yordani?
9. Mbona Elisha alikataa zawadi za Naamani?
10. Gehazi alifanya nini? Nini ilifanyika kwake?

## Majibu

1. Naamani alikuwa nahodha wa jeshi la Shamu.
2. Naamani alikuwa na ukoma.
3. Nabii wa Israeli ataponya Naamani.
4. "Mfalme anafikiri mimi ni Mungu kuponya ukoma?" Alifikiria Mfalme wa Shamu alikuwa anatafuta ugomvi naye.
5. Oga kwa Mto wa Yordani mara 7.
6. Naamani alikasirika. Hakutaka kuoga kwa Mto waYordani.
7. "Kama Elisha angekwambia kufanya kitu kikubwa, ungefanya. Ni rahisi wewe kuoga na upone."
8. Naamani alioga kwa Mto wa Yordani mara 7 na akapona.
9. Mungu aliponya Naamani. Elisha hakuchukua zawadi iliyokuwa ya kazi ya Mungu.
10. Gehazi alidanganya. Alichukua zawadi kutoka kwa Naamani. Alipewa ukoma wa Naamani.



# 74 Naamani

## Kwa Biblia

2 Wafalme mlango wa 5

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima kila mara tuheshimu Mungu. Lazima tufanye sasawa na vile Mungu anasema

## Somo

Naamani alikuwa mtu wa maana sana. Alikuwa nahodha wa jeshi la Shamu. Alikuwa ni mmoja wa watu wa maana wa mfalme. Alikuwa ni mtu mjasiri. Alisaidia nchi yake kushinda vita vingi.

Lakini Naamani alikuwa na ugonjwa mbaya. Alikuwa na ukoma. Ukoma ulikuwa ugonjwa mbaya. Haikuwa na tiba. Naamani angeweza kufa kutokana na ukoma.

Mataifa ya Israeli na Shamu walikuwa maadui. Makundi ya wanajeshi wa Shamu walienda Israeli. Waliuwa watu. Waliiba kutoka kwa Wasraeli. Wakati mwingine waliiba vijana wasichana na wavulana kuwafanya watumwa.

Kijana msichana aliibiwa kutoka kwa kijiji cha Israeli. Aliuzwa kama mtumwa. Mke wa Naamani alinunua huyu kijana msichana kama mtumwa. Huyu msichana hakuwa na furaha kwa kuchukuliwa kutoka kwa familia yao. Lakini alifanyia mke wa Naamani kazi vizuri.

Mke wa Naamani alikuwa na wasiwasi juu ya Naamani. Ukoma wake ulikuwa unaendelea kuwa mbaya. Huyo msichana mtumwa hakupenda mwajiri wake awe na huzuni. Huyo msichana alimwambia, "Kama Naamani angeenda amwona nabii aliye nchi ya Israeli, angemponya huu ukoma wake." Huyu msichana aliambia mke wa Naamani juu ya miujiza yenye Elisha alifanya.

Naamani aliambia Mfalme wa Shamu maneno yenye msichana mtumwa alisema. Mfalme wa Shamu alitaka nahodha wake apone. Aliambia Naamani aende aone nabii Elisha kwa nchi ya Israeli.

Mfalme wa Shamu aliandikia Mfalme wa Israeli barua. Naamani alibeba zawadi nyingi sana. Alibeba fedha, dhahabu na nguo nzuri. Naamani alisafiri kwenda nchi ya Israeli. Alienda kuona Mfalme wa Israeli.

Mfalme wa Israeli alisoma barua kutoka kwa Mfalme wa Shamu. Barua ilisema hivi, "Ninatuma Naamani kwako ili umponye kutoka kwa ukoma." Mfalme wa Israeli alirarua nguo zake. Alikasirika sana. Alisema, "Huyu Mfalme wa Shamu anadhani mimi ni Mungu? Anadhani mimi naweza kuponya Naamani kutoka kwa ukoma? Lazima anataka ugomvi kwangu."

Elisha alisikia kwamba Naamani alikuwa ameenda kwa Mfalme wa Israeli kuponywa ukoma. Elisha alituma ujumbe kwa Mfalme. "Tuma Naamani kwangu. Nitamwonyesha kwamba kuna nabii Israeli."

Naamani alienda kuona Elisha. Alifika kwa nyumba ya Elisha na farasi wake na magari. Elisha alituma  ujumbe kwa Naamani, "Enda uoge kwa Mto wa Yordani mara saba. Halafu utapona."

Naamani alikuwa mtu wa maana sana Shamu. Kila mtu alimwinamia. Walimpea heshima. Naamani alitarajia Elisha ajitokeze na amwone. Alitarajia Elisha afanye muujiza wa ajabu. Naamani alijifunza kuwa mpole. Alijifunza kwamba Mungu ni wa ajabu.

Naamani alikasirika sana. Elisha hakuwa amekuja kumwona. Elisha hakuwa amefanya muujiza wa ajabu. Elisha alikuwa ametuma ujumbe tu. Alimwambia Naamani aende aoge kwa Mto wa Yordani. Naamani alitoka akaenda na gadhabu kuu. Hangeenda kuoga kwa matope ya Mto wa Yordani. Kama angetaka kuoga, angeoga Abana na Farpari mito mikubwa ya Shamu.

Watumishi wa Naamani walimwambia, "Kama Elisha angekwambia ufanye kitu kikubwa, ungekifanya. Ni rahisi sana wewe kuenda uoge na upone." Alisikiliza mawaidha ya watumishi wake.



Naamani alienda kwa Mto wa Yordani. Naamani alienda ndani ya maji ya Mto wa Yordani na akaoga. Alienda ndani ya maji ya mto mara saba akioga. Naamani alipotoka ndani ya maji mara ya saba, alikuwa amepona. Alitii Mungu. Alifanya sasawa na vile Elisha alisema. Kwa hivyo alipona.

Naamani alienda kwa nyumba ya Elisha. Aliambia Elisha, "Sasa najua kwamba Mungu aliye wa kweli ni Mungu wa Israeli." Naamani alimpa Elisha zawadi kama shukrani. Lakini Elisha hakuchukua hiyo zawadi kutoka kwa Naamani. Hakukuwa Elisha ndiye alimponya Naamani. Ilikuwa nguvu za Mungu. Naamani alisema kwamba ataabudu Mungu wa Israeli wa kweli wakati wote. Alianza safari ya kurudi nyumbani Shamu.

Gehazi alikuwa mtumishi wa Elisha. Gehazi aliona zawadi zenye Naamani alikuwa ameleta. Gehazi alifikiria kwamba Elisha angechukua zingine. Gehazi alienda mbiyo kufuata Naamani. Gehazi aliambia Naamani uongo. Alisema kwamba Elisha alihitaji fedha kidogo na nguo nzuri aina mbili. Naamani alimpa Gehazi fedha kidogo na nguo. Gehazi alipeleka nyumbani na kuficha.

Elisha alikuwa nabii wa Mungu. Alijua chenye Gehazi alikuwa amefanya. Gehazi alisema uongo. Alichukua zawadi zilizotakiwa ziwe za Mungu. Elisha alisema kwamba, ukoma wa Naamani utakushika wewe Gehazi kama adhabu.